TANGAZO LA SERIKALI Na. 27 la tarehe 12/1/2024

SHERIA YA UDHIBITI WA USAFIRI ARDHINI,
(SURA YA 413)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya Kifungu cha 41(1)(c))*

KANUNI ZA VIGEZO NA MASHARTI YA KUTOA HUDUMA ZINAZODHIBITIWA ZA MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI ZA MWAKA 2024

## MPANGILIO WA KANUNI

*Kanuni* *Jina*

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA AWALI

1. Jina.
2. Matumizi.
3. Tafsiri.

SEHEMU YA PILI
VIWANGO VYA CHOMBO NA MAHITAJI YA USALAMA

4. Mahitaji ya jumla ya usalama kwa chombo cha kibiashara.
5. Mabadiliko ya chombo.

SEHEMU YA TATU
VIWANGO MAALUM NA MAHITAJI YA USALAMA

6. Viwango na mahitaji ya usalama kwa chombo cha usafiri wa umma.
7. Viwango na mahitaji ya usalama kwa chombo cha kusafirisha mizigo.
8. Viwango na mahitaji ya usalama kwa chombo cha huduma ya usafiri wa kukodi.

SEHEMU YA NNE
VIWANGO VYA UBORA WA HUDUMA

9. Mahitaji ya huduma.
10. Muda wa basi kusimama kituo cha njiani.
11. Mahitaji ya kuwa na wataalam.
12. Matakwa ya kutoa huduma kupitia kampuni au ushirika.

SEHEMU YA TANO
MASHARTI YA JUMLA

13. Adhabu ya jumla.
14. Kumzuia Afisa.
15. Notisi ya kujiondoa kutoa huduma.
16. Mapitio.
17. Kufutwa.

SHERIA YA UDHIBITI WA USAFIRI ARDHINI,
(SURA YA 413)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya Kifungu cha 41(1)(c))*

KANUNI ZA VIGEZO NA MASHARTI YA KUTOA HUDUMA ZINAZODHIBITIWA ZA MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI ZA MWAKA 2024

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

Jina

**1**. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Vigezo na Masharti Ya Kutoa Huduma Zinazodhibitiwa za Mamlaka Ya Udhibiti Usafiri Ardhini za mwaka 2024.

Matumizi

**2**. Kanuni hizi zitatumika kwa vyombo vinavyokusudiwa kutoa huduma za usafirishaji kibiashara Tanzania Bara.

Tafsiri

**3**. Katika Kanuni hizi isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

Sura ya 413

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini;

"Mamlaka" maana yake ni Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini iliyoanzishwa chini ya Sheria;

"Shirika la Viwango" maana yake ni Shirika la Viwango Tanzania lililoanzishwa chini cha Sheria ya Viwango;

"Mkurugenzi Mkuu" maana yake ni Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka aliyeteuliwa kwa mujibu wa Sheria;

"leseni" maana yake ni leseni za kutoa huduma za usafirishaji kwa njia ya barabara zinazotolewa na Mamlaka kwa ajili ya huduma inayodhibitiwa;

"kelele" maana yake ni sauti zenye kadhia kwa binadamu ambazo zinaweza kusababisha madhara hasi kwa afya yake au mazingira;

"bidhaa za kukera" maana yake ni bidhaa zinazoweza kuleta karaha kama vile damu kavu, maiti, nyama ya mnyama aliyekufa, mifupa, samadi, nguo chafu ambazo uchafu wake hautokani na mafuta ya gari, mzoga, mboga zilizooza, mafuvu na viungo vingine vya binadamu;

"mtoa huduma" maana yake ni mmiliki wa leseni ya uendeshaji wa chombo kinachotoa huduma ya usafiri kibiashara;

Sura ya 297

"karakana iliyosajiliwa" maana yake ni karakana iliyokidhi viwango na kusajiliwa na Shirika la Viwango kwa ajili ya utengenezaji wa vyombo vinavyotoa huduma za usafiri kibiashara;

"barabara" maana yake ni barabara kuu, barabara za kawaida, barabara za mitaa, daraja, kalvati, kivuko, maegesho ya magari, njia ya waenda kwa miguu au njia ya hatamu ambapo vyombo vya usafiri vinaweza kupita na umma unaweza ukafika endapo barabara hizo zimezuiwa au vinginevyo kwa masharti yoyote yale isipokuwa barabara gegedu kwenye maeneo ya makazi; na

"chombo" maana yake ni chombo kinachoendeshwa kwa mitambo au umeme kilichokusudiwa kutoa huduma ya usafirishaji kibiashara;

## SEHEMU YA PILI
## VIWANGO VYA CHOMBO NA MAHITAJI YA USALAMA

Mahitaji ya jumla ya usalama kwa vyombo vya kibiashara

**4**.-(1) Mtoa huduma wa chombo cha usafiri kibiashara anapaswa kuhakikisha kuwa-

(a) sakafu ya chombo cha usafiri isiwe ya kuteleza, kushika kutu na chombo kiwe kimetengenezwa katika hali ya kumkinga abiria dhidi ya vumbi, mvuke, mafusho, kelele, hitilafu ya umeme, dutu hatarishi, kuvuja kwa mafuta na vilainishi vingine hatari;

(b) milango na madirisha ya chombo kinachotoa huduma lazima ifunguke na kufunga kwa urahisi na isiruhusu vumbi au maji kuingia sehemu anapoketi abiria;

(c) usukani wa chombo uwe mbele upande wa kulia;

(d) mwamba wa chombo, mineso, ekseli na rimu za vyombo vya usafiri kwa umma viwe vimefungwa madhubuti na havijapasuka wala kuungwa kwa umeme;

(e) chombo hakitaruhusiwa kuendeshwa, kutoa huduma au kuegeshwa barabarani au mahali pengine kama hakijafanyiwa matengenezo pamoja na vifaa vyake;

(f) chombo kisiwe kimeungwa minyororo, vyuma, vifaa, gurudumu au vifaa vingine ndani au nje ya chombo na kuhatarisha maisha ya dereva, wahudumu, abiria na watumiaji wengine wa barabara; na,

(g) chombo kinaendeshwa kwa ajili ya lengo lililokusudiwa.

(2) Mtoa huduma atakayekiuka masharti ya kanuni hii atakuwa ametenda kosa na atakapopatikana na hatia atalipa faini isiyopungua Shilingi laki mbili na isiyozidi Shilingi laki tano au kifungo kisichopungua mwezi mmoja na kisichozidi miezi mitatu jela au vyote.

Mabadiliko ya chombo

**5**.-(1) Mtoa huduma wa chombo kinachotoa huduma ya usafiri kibiashara anaweza kubadilisha chombo chake isipokuwa mabadiliko hayo yanapaswa kufanyika-

(a) kwa kuzingatia vigezo vilivyoainishwa na mtengenezaji na kuidhinishwa na Shirika la Viwango; au

(b) katika karakana iliyothibitishwa na Shirika la Viwango.

(2) Bila kuathiri masharti yaliyoainishwa katika kanuni ndogo ya (1), chombo cha abiria aina ya basi hakitaruhusiwa kuundwa kwenye mwamba wa lori.

## SEHEMU YA TATU
## VIWANGO MAALUMU NA MAHITAJI YA USALAMA

Viwango na mahitaji ya usalama kwa vyombo vya usafiri wa umma

**6**. Mtoa huduma wa chombo cha usafiri wa umma anapaswa kuhakikisha kuwa chombo kinakuwa na nafasi kwa ajili ya kuhudumia abiria wenye mahitaji maalum.

Viwango na mahitaji ya usalama kwa vyombo vya kusafirisha mizigo

**7**. Mtoa huduma wa chombo cha kusafirisha mizigo anapaswa kuhakikisha kuwa-

(a) chombo cha kusafirisha mizigo kimetenganisha sehemu ya dereva na sehemu ya mizigo ili kuzuia mwingiliano baina ya mizigo na dereva; na

(b) mizigo iliyobebwa iwe imefunikwa ili kuzuia kudondosha kwa chembechembe, vumbi, unyevu, kuvuja au moshi.

Viwango na mahitaji ya usalama kwa vyombo vya Huduma ya usafiri wa kukodi

**8**.-(1) Mtoa huduma wa chombo cha usafiri wa kukodi anapaswa kuhakikisha kwamba -

(a) chombo kinakuwa na nafasi kwa ajili ya kuhudumia abiria wenye mahitaji maalum;

(b) abiria hawakai ndani ya chombo wakati chombo kikifanyiwa matengenezo au kujazwa mafuta;

(c) chombo cha usafiri wa kukodi hakibebi wanyama hai, bidhaa hatarishi au zinazokera;

(2) Mtoa huduma atakayekiuka masharti ya kanuni hii atakuwa ametenda kosa na atakapokutwa na hatia-

(a) ikiwa ni pikipiki ya magurudumu mawili au matatu, atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi elfu thelathini lakini isiyozidi shilingi elfu hamsini au kifungo cha muda usiozidi miezi mitatu jela au vyote;

(b) ikiwa ni teksi ya kukodi, atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi elfu thelathini lakini isiyozidi shilingi elfu hamsini au kifungo cha muda usiozidi miezi mitatu jela au vyote;

(c) ikiwa ni mtoa huduma wa teksi mtandao, atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi elfu hamsini lakini isiyozidi shilingi laki moja au kifungo cha muda usiozidi miezi mitatu jela au vyote; au

(d) ikiwa ni mtoa huduma wa teksi mtandao wa kushirikiana, atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi laki tano lakini isiyozidi shilingi milioni moja au kifungo cha muda usiozidi miezi mitatu jela au vyote.

## SEHEMU YA NNE
## VIWANGO VYA UBORA WA HUDUMA

Mahitaji ya huduma
T.S Na. 76 la 2020
T.S Na. 77 la 2020
T.S Na. 78 la 2020

**9.** Mtoa huduma atahakikisha kuwa chombo cha huduma ya biashara kinakidhi mahitaji yaliyoainishwa chini ya Kanuni za leseni za Usafirishaji za Vyombo vya Huduma za Usafiri wa Umma, Kanuni za leseni za Usafirishaji za Vyombo vya Huduma za Usafirishaji wa Mizigo, na Kanuni za leseni za Usafirishaji za Vyombo vya Huduma za Usafiri wa Kukodi.

Muda wa basi kusimama kituo cha njiani

**10**. Mtoa huduma atahakikisha chombo cha biashara hakisimami kituo cha njiani kwa zaidi ya muda wa dakika tatu.

Takwa la kuwa na wataalamu

**11**.-(1) Mtoa huduma anayemiliki vyombo vya usafiri visivyozidi sita anawajibika kuwa na angalau mtaalam mmoja mwenye stashahada ya masuala ya usimamizi wa logistiki na uchukuzi kutoka katika Chuo kinachotambulika.

(2) Mtoa huduma anayemiliki idadi ya vyombo vya usafiri sita au zaidi anawajibika kuwa na angalau mtaalam mmoja mwenye stashahada ya masuala ya usimamizi wa logistiki na uchukuzi na mwajiriwa wa kudumu mwenye stashahada ya ufundi wa magari kutoka katika Chuo kinachotambulika.

(3) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1) na (2), mtoa huduma anapaswa kuajiri dereva aliyethibitishwa na mhudumu aliyesajiliwa na Mamlaka.

Matakwa ya kutoa huduma kupitia kampuni au ushirika

**12**.Mtoa huduma anayehitaji kutoa huduma kwenye njia zenye umbali wa zaidi ya kilomita mia sita anapaswa-

(a) kumiliki vyombo vya usafiri visivyopungua vinne; na

(b) kutoa huduma kupitia kampuni au ushirika.

## SEHEMU YA TANO
## MASHARTI YA UJUMLA

Adhabu ya jumla

**13**. Mtu atakayekiuka masharti ya Kanuni hizi atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani pale ambapo hakuna adhabu maalum iliyotolewa, atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi laki mbili lakini isiyozidi shilingi laki tano au kifungo cha muda usiopungua miezi mitatu lakini usiozidi mwaka mmoja au vyote kwa pamoja.

Kumzuia Afisa

**14.** Mtu anayezuia Afisa wa Mamlaka au Afisa wa Polisi kutekeleza majukumu yake chini ya Kanuni hizi anatenda kosa.

Notisi ya kujiondoa kutoa huduma

**15**. Mtoa huduma anayekusudia kuacha kutoa huduma za usafirishaji kibiashara atatakiwa kutoa notisi ya maandishi ya mwezi mmoja kwa Mamlaka kabla ya kujiondoa.

Mapitio TS. Na. 73 la 2020

**16**. Mtu ambaye hataridhishwa na maamuzi ya Mamlaka atatakiwa kuwasilisha maombi ya mapitio kwa mujibu wa Kanuni za Utaratibu wa Mapitio za Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini.

Kufutwa T.S. Na. 412 la 2014

**17**.Kanuni za Vigezo na Masharti ya Kutoa huduma za SUMATRA zinafutwa.

Dodoma,
2 Disemba, 2023

AHMED MOHAMED AME,
*Mwenyekiti wa Bodi*